

HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA

BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA

Simu Namba: 023 2410210
: 023 2410251
Faksi Namba: 023 2410211
Barua Pepe:ded@newaladc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Wilaya ya Newala,
Sanduku La Posta 16,
NEWALA – MTWARA.

Kumb. Na. NDC/I.20/II/VOL.III/179

13/11/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala amepokea Kibali cha Ajira Mbadala toka kwa Katibu Mkuu OR – Utumishi chenye Kumb. Na. FA.170/362/01'A'/54 cha tarehe 8/10/2020, hivyo anapenda kuwatangazia watazania wote wenye sifa kutuma maombi kama ifuatavyo:-

1. MTENDAJI WA KIJIKI III – NAFASI 4

SIFA ZA MWOMBAJI

- Mwombaji awe raia wa Tanzania.
- Mwombaji awe na akili timamu.
- Awe amehitimu elimu ya kidato cha Nne au Sita.
- Awe amehitimu Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo – Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI ZA KUFANYA

1. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa serikali ya Kijiji;
2. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji;
3. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji;
4. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji;

4. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji;
5. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu;
6. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji;
7. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbumbu zote na nyaraka za Kijiji;
8. Kusimamia ugatuaji wa Sheria Ndogo za Kijiji na
9. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

NGAZI YA MSHAHARA

Atakayefaulu usajili na kuajiriwa atalipwa mshahara ngazi ya TGS B₁ kwa mwezi.

TARATIBU ZA KUTUMA MAOMBI

1. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono na iambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu, taaluma na CV (Curriculum Vitae), cheti cha kuzaliwa na picha moja ya passport size ya hivi karibuni.
2. Barua iandikwe namba za simu za mwombaji za kiganjani.
3. **Mwombaji awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45**
4. Kwa walioajiriwa maombi yapitishwe na Waajiri wao wa sasa.
5. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 26/11/2020 saa 9: 30 Alasiri siku ya Alhamisi.
6. Waombaji waandike majina yao yote matatu kwa kirefu.

Barua za maombi ya kazi zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Newala,
Sanduku la Posta 16,
NEWALA.

Tangazo limetolewa na



Duncan G. Thebas
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA

MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA YA NEWALA